



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UBORESHAJI WA

DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 74 (6) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ina jukumu la kuandikisha Wapiga Kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara. Tume hivi sasa ipo katika utekelezaji wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ikiwa ni maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Zoezi la uboreshaji wa Daftari limegawanyika katika *Routes*, ambapo kwa sasa zoezi liko kwenye *Route* ya kumi (10) ambayo inajumuisha mikoa ya Njombe na Ruvuma kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar (Unguja na Pemba). Uboreshaji kwenye maeneo tajwa ulipangwa kufanyika kwa siku saba (7) kuanzia tarehe 30 Desemba 2019 hadi tarehe 05 Januari 2020.

Hata hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imesogeza mbele kuanza kwa zoezi hilo kwa muda wa siku mbili kwa mikoa ya Njombe na Ruvuma ambapo zoezi hilo sasa litafanyika kuanzia tarehe 01 Januari hadi tarehe 07 Januari 2020.

Aidha, mabadiliko haya hayatahusu zoezi la uboreshaji wa Daftari kwa Tanzania Zanzibar ambako zoezi hilo litafanyika kama ilivyopangwa yaani kuanzia tarehe 30 Desemba 2019 hadi 05 Januari 2020.

Uboreshaji huu unawahusu Raia wa Tanzania ambao wametimiza umri wa miaka 18 na wale ambao watatimiza umri wa miaka 18 siku ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka ujao (2020). Pia, unahusisha wale ambao wamehama kutoka maeneo yao ya awali na kuhamia maeneo mengine ya Uchaguzi na wale ambao Kadi zao zimeharibika au kupotea na wale ambao wanatakiwa kuondolewa kwenye Daftari kama waliofariki na waliopoteza sifa.

Aidha zoezi hili ambalo lilizinduliwa tarehe 18 Julai 2019 Mkoani Kilimanjaro linaendelea vizuri na tayari limeshafanyika kwenye mikoa 17. Mikoa ambayo imekamilisha zoezi hilo ni pamoja. na Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Simiyu, Mara, Mwanza, Kigoma, Tabora, Songwe, Kagera, Geita, Shinyanga, Katavi, Rukwa, Singida, Dodoma, Iringa na Mbeya.

“Kadi yako, Kura yako. Nenda Kajiandikishe”

Imetolewa na:



Abdulwakil Saiboko

Afisa Habari Mwandamizi

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

29.12.2019